TANGAZO LA SERIKALI NA.599 la tarehe 25/12/2015

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

SHERIA NDOGO.

(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 153)

SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOGWE, 2015

SEHEMU YA I

UTANGULIZI

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (uanzishaji Mfuko wa Afya ya Jamii) Wilaya ya Mbogwe, 2015 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo:-

"Ada ya Mtumiaji" maana yake ni malipo anayolipa mtumiaji wa huduma kwa Hospitali, Kituo cha Afya au Zahanati,kwa mwaka kwa ajili ya Huduma ya Afya iliyotolewa kwa mtumiaji;

"Asasi' ni pamoja na Shule, Vyuo, Vikundi mbalimbali vilivyosajiliwa kwa mujibu wa sheria au vikundi vyovyote vilivyokubaliwa na kuidhinishwa na Bodi;

"Bodi" maana yake ni chombo kinachosimamia Huduma za Afya za Halmashauri;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe;

"Huduma za afya" maana yake ni huduma zote za afya zinazotolewa na Hospitali za Serikali na watu binafsi,na zinajumuisha huduma nyingine za afya zilizoanzishwa kwa madhumuni ya kutoa huduma za afya ikiwa ni pamoja na Vituo vya Afya na Zahanati;

"Kadi" maana yake ni kitambulisho kinachotolewa kwa mwanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii;

"Kituo cha Huduma kilichoteuliwa" maana yake ni kituo kinachotoa Huduma za Afya na ni pamoja na kituo chochote kilichoanzishwa au kinachoendeshwa kwa malengo ya kutoa Huduma za Afya kinachomilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe, Serikali, Asasi ya Kidini, Mtu au Watu binafsi ambacho kinahusika na Mfuko wa Afya ya Jamii;

"Mchango" maana yake ni malipo ya fedha ya hiari, yatakayotolewa na mwanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii;

"Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya", maana yake ni Daktari ambaye ni Msimamizi Mkuu wa shughuli zote za huduma za Afya katika Halmashauri ya Wilaya.

"Mwanachama" maana yake ni mtu yeyote ambaye anachangia Huduma za Afya ya Jamii;

"Malipo ya Huduma" maana yake ni malipo yanayolipwa katika kituo cha kutolea Huduma za Afya kwa wasio wanachama wa Mfuko. (Papo kwa Papo)

"Wizara" maana yake ni Wizara yenye dhamana ya masuala ya Afya na Ustawi wa jamii.

SEHEMU YA II
MFUKO WA AFYA YA JAMII

Mfuko wa Afya ya Jamii

4.(1) Kutakuwa na Mfuko wa Afya ya Jamii ambao ni Mfuko wa hiari wenye lengo la kutoa huduma za Afya, ambapo mwanachama atakuwa akilipia huduma hizo na Serikali itatoa mchango wake wa fedha kama jazilio sawia kwa mchango kutoka kwa

mwanachama;

(2) Matumizi ya fedha yatafanywa na kusimamiwa na Bodi pamoja na timu ya uendeshaji wa huduma za Afya ya Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Madhumuni ya Mfuko

5. Madhumuni ya Mfuko yatakuwa ni:-

(a) Kutafuta vyanzo vya fedha kutoka katika jamii kwa ajili ya kutoa huduma bora za Afya kwa wanachama;

(b) Kutoa huduma bora za Afya zinazopatikana kwa kutumia mipango endelevu; na

(c) Kuboresha huduma za Afya katika jamii kwa kugawanya madaraka na kuzipa nguvu jamii katika kufanya maamuzi na kuchangia katika masuala yanayohusu Afya zao.

Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii

6.-(1) Kutakuwa na Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii wa Halmashauri ambaye atateuliwa na Mkurugenzi wa Halmashauri baada ya kupokea mapendekezo kutoka Timu ya Uendeshaji ya Halmashauri.

(2) Majukumu ya Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii yatakuwa kama ifuatavyo:-

a) Kufuatilia, kusimamia na kuratibu uendeshaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii kwenye vituo vya kutolea Huduma za Afya ya Jamii;

b) Kuwa kiungo kati ya Halmashauri ya Wilaya,Jamii na Wadau mbalimbali kwa ushirikiano na mhasibu wa Mfuko; na

c) Kuandaa taarifa za Mfuko wa Afya ya Jamii za robo, na mwaka pamoja na majukumu mengine atakayopangiwa na Halmashauri.

Muundo wa Bodi.

7 (1) Bodi itakuwa na wajumbe wafuatao:-

a) Wawakilishi wanne wa watumiaji Huduma za Afya, kati yao wawili ni lazima wawe ni wanawake;

(b) Mwakilishi mmoja kutoka watoa huduma za Afya bila faida na Mwakilishi mmoja kutoka watoa huduma za afya binafsi kwa faida waliochaguliwa na Halmashauri ya wilaya kutoka vituo vya kutoa huduma za afya ambavyo tayari vina Mkataba wa kutoa huduma za Afya na Bodi;

(c)Mwenyekiti wa kamati ya Elimu, Afya na Maji;

d)Afisa Mipango wa Wilaya;

(e) Mganga Mkuu wa Wilaya ambae atakuwa katibu wa Bodi;

(f) Mwakilishi Mmoja kutoka Hospitali; na

(g)Mwakilishi mmoja kutoka timu ya uendeshaji wa huduma za Afya za Mkoa.

(2) Wataalamu ambao hawatapiga kura:-

(a) Afisa Mipango wa Wilaya ;

(b) Mganga Mkuu wa Halmashauri ambaye atakuwa Katibu wa Bodi;

(c) Mwakilishi mmoja kutoka Hospitali ya Halmashauri, endapo hakuna atatoka kwenye hospitali teule; na

(d) Mwakilishi mmoja kutoka Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya

Mkoa.

Mwenyekiti wa Bodi atachaguliwa miongoni mwa Wajumbe waliotajwa katika (1) (a) – (c) hapo juu.

Sifa za Wajumbe wa Bodi.

8. Mjumbe wa Bodi atakuwa na sifa zifuatazo:-

(a) Awe Raia wa Tanzania, sharti hili halitawahusu wajumbe kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali;

(b) Awe na umri usiopungua miaka ishirini na moja na kuendelea;

(c) Awe amehitimu Elimu ya Sekondari na kuendelea;

(d) Awe na uzoefu na amewahi kuonyesha uwezo wake wa kuongoza katika shughuli za huduma ya jamii;

(e) Awe na akili timamu;

(f) Asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai;

(g) Asiwe na wadhifa wowote wa kisiasa kupitia chama chochote cha siasa isipokuwa kwa wale wanaoingia kwa nyadhifa zao;

(h) Awe mwanachama hai wa Mfuko wa Afya ya Jamii.

(i) Mjumbe wa kuchaguliwa awe Mkazi wa Halmashauri;

Majukumu na Kazi za Bodi.

9. (1) Ili kufanikisha malengo yake makuu, Bodi itakuwa na kazi zifuatazo:-

(a) Itasimamia masuala na shughuli zote zinazohusu Mfuko wa Afya ya Jamii;

(b) Kusimamia Huduma za Afya katika Halmashauri;

(c) Kushauriana na Timu ya Uendeshaji ya Huduma za Afya ya Halmashauri na kuhakikisha kuwa Huduma ya Afya ni

bora na ya kitaalamu;

(d) Kukusanya na kusimamia mapato ya Mfuko wa Afya ya Jamii;

(e) Kupendekeza kwa Halmashauri watu wanaostahili kusamehewa kutoa mchango kwenye Mfuko;

(f) Kuweka malengo ya Mfuko;

(g) Kupitia ripoti na taarifa kutoka Kamati ya Afya ya Kata au chanzo kingine chochote;

(h) Kuratibu makusanyo, matumizi na kudhibiti mapato; na

(i) Kushiriki kupanga Mipango ya Afya ya mwaka kwa ajili ya kuthibitishwa na Halmashauri.

(2) Bodi katika kutekeleza majukumu yake, itapokea na kutekeleza maagizo ya Halmashauri kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu.

Muda wa kukaa Madarakani

10. (1) Mjumbe wa Bodi atakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe ya uzinduzi wa Bodi na anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu tu.

(2) Endapo nafasi yoyote ya Mjumbe wa Bodi itaachwa wazi kwa sababu ya kifo, kujiuzulu au kwa sababu nyingine yoyote ile, Mjumbe mwingine atachaguliwa kujaza nafasi hiyo iliyoachwa wazi.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2), haitaruhusiwa kuchagua mjumbe mwingine iwapo kipindi kilichobaki ni chini ya miezi sita.

Akaunti ya Mfuko

11. (1) Kutakuwepo na Akaunti Maalum au Akaunti nyingine itakayoteuliwa na Serikali itakayotumika na Halmashauri ambayo fedha zote zitakazokusanywa kwa ajili ya Mfuko zitahifadhiwa na kutolewa;

(2) Waidhinishaji kwenye hundi za Mfuko watakuwa kama ifuatavyo:-

a. Mwenyekiti wa Bodi na Mjumbe mmoja wa Bodi ambao watakuwa Kundi "A"; na

b. Katibu wa Bodi ambaye atakuwa ni Mganga Mkuu wa Halmashauri na Mweka Hazina wa Halmashauri ambao watakuwa Kundi "B"

(3) Kila baada ya miezi mitatu, Bodi itakuwa inapitia na kutoa taarifa ya Akaunti ya Mfuko na kuiwasilisha kwa Halmashauri.

(4) Akaunti Maalumu itakaguliwa na Wakaguzi waliochaguliwa kwa mujibu wa Kanuni za Fedha za Serikali.

Matumizi ya Fedha za Mfuko

12 Fedha zitakazokusanywa na Mfuko zitatumika kwa madhumuni yafuatavyo:-

(a) Masuala yanayohusiana na Afya yaliyotajwa katika mpango kabambe wa afya wa Halmashauri na kuidhinishwa na Halmashauri; na

(b) Suala au shughuli yoyote muhimu ya Afya itakavyoonekana inafaa na kama itaidhinishwa na Bodi.

(c) Asilimia 80 ya Mapato itabaki kwenye Akaunti Maalumu na Asilimia 20 itarudi kwenye vituo kwa ajili ya matumizi ya vituo.

Vyanzo vya

13. Vyanzo vya mapato ya Mfuko vitatokana na:-

Mapato

a) Fedha zote zitakazopokelewa kutokana na Michango ya Wanachama;

b) Ruzuku kutoka kwenye Halmashauri na Serikali Kuu;

c) Wahisani mbalimbali toka ndani na nje ya Halmashauri;

d) Michango ya watu binafsi wanaoishi ndani na nje ya Halmashauri;

e) Ada za watumiaji Papo kwa Papo;

f) 10% ya ushuru utakaotozwa na Halmashauri kutoka vyanzo mbalimbali itatengwa kwa ajili ya Mfuko;

g) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; na

h) Fedha zozote halali ambazo Mfuko unaweza kupata toka mahali pengine popote.

Mipango

14. (1) Miezi miwili kabla ya kuanza kwa mwaka wa Fedha wa Serikali, Bodi itapitia mipango na Bajeti ya mwaka inayoonyesha kiwango kinachotarajiwa kupatikana na mgawanyo wa fedha kwa ajili ya utoaji huduma za Afya na maendeleo katika maeneo ya Halmashauri.

(2) Bodi itapokea, itajadili, itachambua na kuidhinisha Mpango wa Afya na kuwasilishwa kwa Halmashauri kwa ajili ya kuidhinishwa kwa kupitia Kamati za Halmashauri.

(3) Bodi itatoa maoni ya Bajeti ya nyongeza kama kutakuwa na haja ya kufanya hivyo na kama mazingira yataruhusu.

(4) Mipango ya Bajeti ya Mfuko itaandaliwa

kulingana na utaratibu kama ilivyoainishwa katika vifungu vidogo vya (1) na (2) hapo juu, ambayo ni lazima iwasilishwe kwa Halmashauri kwa ajili ya kuidhinishwa.

Usimamizi wa Mfuko

15. Usimamizi na Uendeshaji wa Mfuko utakuwa chini ya:-

(a) Halmashauri kupitia Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri katika ngazi ya Wilaya;

(b) Kamati ya Maendeleo ya Kata kupitia Kamati ya Afya ya Kata katika ngazi na Kamati ya Kituo cha Afya iwapo kutakuwa na Kituo cha Afya katika ngazi ya kata;

(c) Kamati ya Serikali ya Kijiji kupitia Kamati ya Zahanati katika ngazi ya kijiji.

Taarifa ya Fedha

16. Mwezi mmoja baada ya mwaka wa Fedha wa Serikali, Bodi itatakiwa kupokea na kupitia Taarifa ya Mapato na Matumizi ya Fedha na kuwasilisha kwa Halmashauri.

SEHEMU YA III
KAMATI YA AFYA YA KATA

Kamati ya Afya ya Kata

17. Kutakuwa na Kamati ya Afya ya Kata.

Wajumbe wa Kamati ya Afya ya Kata

18. (1) Kamati ya Afya ya Kata itakuwa na Wajumbe wafuatao:-

(a) Diwani anayewakilisha Kata husika;

(b) Afisa Mtendaji wa Kata;

(c) Mwalimu Mkuu mmoja kutoka kwenye Shule ya Msingi ambayo ipo kwenye Kata husika;

(d) Wajumbe wawili watakaowakilisha jamii husika ambapo mmoja wao ni lazima awe Mwanamke;

(e) Tabibu Mfawidhi au Tabibu Mfawidhi Msaidizi; wa kituo cha Afya au Zahanati, ambaye atakuwa Katibu wa Kamati;

(f) Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Kamati ya maendeleo ya Kata kutokana na watu waliopendekezwa Halmashauri za Vijiji zilizomo ndani ya eneo la kata; na

(g) Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata kutoka kwenye vyama vya kijamii kutoka kwenye Kata.

(2) Mwenyekiti wa Kamati ya Afya ya Kata atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe.

(3) Endapo Kamati ya Afya ya Kata itashindwa kutekeleza kazi zake, Bodi itatoa onyo au kuivunja na Halmashauri itafanya utaratibu wa uchaguzi wa wajumbe wengine katika muda usiozidi miezi mitatu (3).

Kazi na Majukumu ya Kamati ya Afya ya Kata

19. (1) Kamati ya Afya ya Kata itakuwa na majukumu yafuatayo:-

(a) Kuhamasisha na kuandaa jamii kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii;

(b) Kuandaa orodha na kuratibu idadi ya Wanachama wa Mfuko wa Afya wa Jamii;

(c) Kusimamia ukusanyaji wa michango ya Mfuko;

(d) Kuratibu viwango vya uchangiaji kwenye Huduma za Afya;

(e) Kupitia Utendaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii na kutoa mapendekezo na ufumbuzi kwa Halmashauri kupitia Bodi ya Afya;

(f) Kuanzisha na kuratibu Mipango ya Afya ya Jamii; na

(g) Kuendesha mikutano ya wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii ndani ya Kata.

(2) Kamati ya Afya ya Kata, itakaa kila baada ya miezi mitatu (3) na Katibu atatoa taarifa ya maandishi siku saba (7) kabla ya siku ya Kikao. Isipokuwa likitokea jambo la dharura.

Utoaji wa Huduma za Afya.

20. Kila mwanachama:-

a) Atakuwa na haki ya kisheria kupata Huduma ya Afya aliyolipia kabla ya kuugua ndani ya eneo la Halmashauri au eneo lingine lolote kwa kadri itakavyo kubaliwa;

b) Atakuwa na haki ya kutoa mapendekezo kuhusu Huduma za Afya kupitia Kamati husika ambayo yatafanyiwa kazi na Bodi; na

c) Atashirikishwa kikamilifu katika uandaaji na utekelezaji wa Mpango wa upatikanaji wa Huduma za Afya katika eneo la Halmashauri.

SEHEMU YA IV
KAMATI YA KITUO CHA AFYA

Kamati ya kituo cha afya

21. (1) Kutaanzishwa katika kila kituo cha afya kamati ya kituo cha afya ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Wajumbe watatu wenye tabia nzuri waliochaguliwa kutoka katika wanachama wanaotumia huduma za afya za jamii au wajumbe

waliosajiliwa kupokea huduma kutoka Hospitalini;

(b) Mjumbe mmoja aliyeteuliwa na vyama visivyo vya serikali(NGOs) vinavyotoa huduma za afya katika eneo;

(c) Mkuu wa kituo cha afya ambaye atakuwa katibu;

(d) Mjumbe mmoja aliyeteuliwa kutoka sekta binafsi inayotoa huduma ya afya bila faida katika eneo;

(e) Wajumbe wawili kutoka kamati za zahanati ambao watachaguliwa kila mwaka;

(f) Mjumbe mmoja kutoka katika kamati za maendeleo za kata (WDC) watakaochaguliwa kila mwaka;

(2) Kamati ya kituo cha afya inaweza kumkaribisha mtu yeyote kutoa utaalam na msaada mwingine, lakini mtu huyo hatakuwa mtoa maamuzi ya mwisho ya kamati.

(3) Walau theluthi moja ya wajumbe wote watakuwa wanawake.

Sifa za wajumbe wa kamati ya kituo cha afya

22. Mtu atateuliwa kuwa mjumbe wa kamati ya kituo cha afya atakuwa na sifa zifuatazo:-

(a) Awe ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na suala la uraia halitahusiana na uwakilishi wa vyama visivyo vya serikali (NGOs) au vyama vya hiari;

(b) Awe na umri wa miaka 21 na sio zaidi ya miaka 65;

(c) Ni mkazi wa eneo ambalo Halmashauri ina mamlaka;

(d) Anaweza kusoma na kuandika Kiswahili;

(e) Hana cheo chochote katika masuala ya siasa.

Vikao vya kamati

23. (1) Kamati itakuwa na vikao vya kawaida kwa uendeshaji wa shughuli zake walau mara moja kila baada ya miezi mitatu;

(2) Mwenyekiti wa kamati ataitisha kikao maalumu au kisicho cha kawaida cha kamati na kueleza

madhumuni ya kikao hicho baada ya kupokea maombi ya maandishi yaliyosainiwa na wajumbe wa kamati wasiopungua theluthi moja.

(3) Katibu atamwarifu kila mjumbe kwa maandishi juu ya sehemu siku na muda wa kikao na shughuli inayotakiwa ifanyike kwa kipindi kisichopungua masaa 24 kabla ya muda wa kikao.

Kazi za kamati ya kituo cha afya

24. Kamati ya kituo cha afya itakuwa na kazi zifuatazo:-

(a) Kupokea na kujadili taaifa za utekelezaji zilizotayarishwa na timu ya wataalam kutoka kituo cha afya;

(b) Kutambua na kutafuta pesa kwa uendeshaji wa kituo cha afya;

(c) Kuwasiliana na Bodi ya huduma ya afya ya Halmashauri na washiriki wengine katika utoaji na uboreshaji wa huduma katika eneo;

(d) Kufanya miundo ya afya endelevu na usambazaji wa madawa na ubadilishaji wa vifaa na watumishi unaowezekana;

(e) Kushauri na kupendekeza kwa Bodi ya huduma za afya ya Halmashauri katika maendeleo ya watu juu ya kuajiri, kutoa motisha ya mafunzo katika kituo cha afya;

(f) Kuwezesha miundombinu ya kutosha ya kituo cha afya;

(g) Kuangalia upatikanaji na usambazaji wa madawa muhimu kemikali na vifaa vya afya.

Kuwajibika kwa kamati

25. Kamati ya kituo cha afya itawajibika kwa Bodi ya huduma ya afya ya Halmashauri.

Vyanzo vya mapato

26. (1) Fedha na vyanzo vya mapato ya kituo cha afya vitakuwa vifuatavyo:-

(a) Michango ya jamii;

(b) Wafadhili au michango ya washirika;

(c) Ruzuku kutoka serikalini;
(d) Ruzuku kutoka Halmashauari;
(e) Chanzo chochote halali.

(2) Fedha zitawekwa katika akaunti na itasimamiwa na kuongozwa na Mganga Mkuu wa Wilaya.

Wajibu wa Kamati ya kituo cha afya

27. (1) Katika ufanyaji wake kazi za kamati kituo cha afya:-
(a) Itahakikisha matakwa ya jamii yanatekelezwa;
(b) Itatafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali;
(c) Itatunza na kuweka kumbukubu za wachangiaji wa mfuko wa afya;
(d) Itaendeleza na kuimarisha ushiriki (partnership) kwa mahusiano uunganishaji na mwingiliano na sekta nyingine katika eneo;
(e) Itahakikisha kwamba kamati ya kituo cha afya inawakilishwa katika Bodi ya huduma ya afya ya Halmashauri.

(2) Timu ya wataalam wa afya wa Halmashauri itatoa ushauri wa kiufundi kwa Timu ya wataalam wa kituo cha afya;
(3) Kamati za kituo cha afya zitawasilisha taarifa za maendeleo kwa Bodi ya huduma ya afya ya Halmashauri kila robo mwaka na nusu mwaka.

Kuvunjwa kwa kamati

28. (1) Endapo kamati ya kituo cha afya itashindwa kutimiza malengo yake kama yalivyoonyeshwa katika hati hii, Halmashauri kamati na kupanga uteuzi wake ndani ya kipindi cha miezi mitatu;

(2) Kwa kipindi chote ambacho hakutakuwa na kamati ya wataalam wa kituo cha afya, Halmashauri itaipa uwezo wa kamati Timu ya wataalm wa kituo cha afya.

SEHEMU YA V
KAMATI YA ZAHANATI

Kamati ya zahanati

29. Kutakuwa na kamati itakayojulikana kama kamati ya zahanati.

Taratibu za kuwapata wajumbe

30.-(1) Kamati ya zahanati itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Wajumbe wa kuchaguliwa watakaokuwa wapiga kura kama ifuatavyo:-

(i) Wajumbe watatu kutoka katika jamii inayotumia zahanati;

(ii) Mwakilishi mmoja kutoka katika vyama visivyo vya kiserikali vinavyotoa huduma ya afya bila faida;

(iii) Mwakilishi mmoja kutoka katika watoa huduma ya afya binafsi kwa faida;

(b) Kutakuwa na sekretarieti ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(i) Mtaalam mmoja kutoka kwenye vyama visivyo vya kiserikali vinavyotoa huduma ya afya bila faida;

(ii) Mwakilishi mmoja kutoka kamati za serikali ya mtaa;

(iii) Mganga mfawidhi wa zahanati ambaye atakuwa katibu, pale ambapo kutakuwa na zahanati zaidi ya moja, kutakuwa na utaratibu wa kupeana zamu.

(2) Idadi ya wajumbe wanawake itakuwa si chini ya theluthi moja ya wajumbe wote.

(3). Mwenyekiti wa kamati ya zahanati atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe walioelezwa

kwenye kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

(4). Wajumbe wa sekretarieti hawatakuwa na haki ya kupiga kura.

Utaratibu wa kuchagua wajumbe.

31.-(1) Wajumbe wa kamati ya zahanati watachaguliwa kwa kufuata utaratibu ufuatao:-

(a) Afisa mtendaji wa kata atatangaza nafasi wazi;

(b) Mapendekezo ya majina ya wagombea yatawasilishwa kwenye timu ya wataalm ya kata ambapo yatachaguliwa kabla ya kuwasilishwa kwenye kamati ya maendeleo ya kata;

(c) Kamati ya maendeleo ya kata itapendekeza majina ya wajumbe na kuyawasilisha kwenye Halmashauri kupitia Bodi ili kuidhinishwa.

Vikao vya kamati ya zahanati

32. (1) Kamati ya zahanati itafanya vikao vyake vya kawaida kila baada ya miezi mitatu, isipokuwa inaweza kuitishwa kikao cha dharura pale itakapohitajika;

(2) Akidi ya mkutano itakuwa ni nusu ya wajumbe wote wa kuchaguliwa ikiwa ni pamoja na mwenyekiti na katibu;

(3) Taarifa ya kikao itatolewa kwa maandishi na Katibu siku saba (7) kabla ya siku ya kikao.

Sifa za mjumbe wa kamati ya zahanati

33. Mtu atakuwa mjumbe wa kamati ya zahanati akiwa na sifa zifuatazo:-

(a) Awe na umri wa miaka ishirini na moja (21) na zaidi;

(b) Awe na elimu ya msingi au zaidi na anajue kusoma na kuandika;

(c) Awe raia wa Tanzania na ni mkazi wa eneo husika. Hata hivyo suala la uraia halitahusisha wawakilishi binafsi au vyama visivyo vya kiserikali;

(d) Asiwe na wadhifa wa kisiasa kutoka chama chochote cha siasa;

(e) Asiwe ametiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai;

(f) Anawakilisha watumiaji wa zahanati.

Kazi na majukumu ya kamati ya zahanati

34. Kamati ya zahanati itakuwa na kazi na majukumu yafuatayo:-

(a) Kuhakikisha kwamba jamii katika eneo la mamlaka yake inapata huduma bora na rahisi za afya;
(b) Kupokea, kujadili na kupitisha mipango na bejeti ya zahanati;
(c) Kujadili utekelezaji wa taarifa zilizoandaliwa na Timu ya wataalam wa zahanati;
(d) Kutafuta na kubainisha vyanzo vya mapato ya kuendeshea huduma za Afya kwenye zahanati;
(e) Kushirikiana na kamati nyingine za afya na mashirika katika utoaji na uboreshaji wa huduma za afya;
(f) Kuendeleza miundo mbinu endelevu ya afya na mgao wa uhakika wa mahitaji muhimu;
(g) Kushauri na kupendekeza kuhusu masuala ya watumishi yanayohusu ajira, mafunzo mgawanyo na motisha;
(h) Kusaidia na kuwezesha timu ya uendeshaji wa zahanati katika kupanga na kusimamia shughuli mbalimbali za jamii katika eneo lake kwa kuzingatia mpango wa maendeleo ya kata;
(i) Kuwasilisha mipango yake ya robo mwaka, nusu mwaka na ya mwaka mzima kwenye Bodi ya huduma za afya ya Halmashauri;
(j) Kufanya mambo mengine muhimu kama itakavyoagizwa na kamati ya maendeleo ya kata.

Uhusiano na sekta nyingine

35. Ili kuboresha utendaji kazi, kamati itakuwa na mhusiano na sekta nyingine kama ifuatavyo:-

(a) Itahakikisha kuwa jamii inawakilishwa na wajumbe kwenye kamati ya zahanati ili kuhakikisha kuwa mahitaji ya jamii yanashughulikiwa;
(b) Itapewa ushauri wa kitaalam na timu ya uendeshaji wa Huduma ya afya ya Halmashauri;
(c) Itawakilishwa kwenye kamati ya kituo cha cha afya kwa mtindo wa kupokezana ili kuhakikisha kuwa mambo ya zahanati yanazingatiwa;
(d) Itashirikiana na wadau wengine kwa kutafuta mapato kujenga na kuimarisha uhusiano.

Vyanzo vya fedha za kamati ya zahanati

36. (1) Vyanzo vya fedha kwa kamati ya zahanati zitahusisha lakini siyo pekee kwa vifuatavyo:-
(a) Michango ya jamii;
(b) Mfuko wa afya ya jamii;
(c) Ruzuku kutoka Halmashauri;

(d) Fedha kutoka kwa wahisani na washirika;
(e) Ruzuku kutoka serikali kuu;
(f) Mfuko wa bima ya afya;
(g) Gharama ya dawa/vifaa tiba kwa asilimia hamsini (50%);
(h) Vyanzo vingine halali vya mapato.

(2) Bila kuathiri kifungu kidogo cha 1 (b) hapo juu ambacho mapato yake anasimamiwa na Bodi ya mfuko wa Jamii, mapato mengineyo ya zahanati yatahifadhiwa katika akaunti ya zahanati na kusimamiwa na Mganga Mfawidhi wa zahanati.

Muda wa kukaa madarakani

37. (1) Wajumbe wote wa Bodi na kamati zote za Afya watakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya ufunguzi na wataondoka madarakani baada ya muda huo lakini wanaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu. Isipokuwa kwa wale wajumbe ambao watashika nafasi zao kwa kupokezana ambao watakaa kwa muda wa mwaka mmoja.

(2) Kama Bodi au mjumbe yeyote wa kamati ya fya anataka kujiuzulu, mjumbe huyo ataweka katika maandishi lengo lake kwa kipindi cha mwezi mmoja kwa Katibu wa Bodi ya Kamati ya afya.

(3) Endapo nafasi yoyote ya mjumbe wa kamati ya zahanati itaachwa wazi kwa sababu ya kifo, kujiuzulu au ulemavu utakomfanya ashindwe kushiriki kikamilifu kama mjumbe au kwa sababu nyingine yoyote ile, mjumbe mwingine atateuliwa kuziba nafasi hiyo na Halmashauri ndani ya kipindi cha miezi mitatu, kufatia mapendekezo kutoka kamati ya maendeleo ya kata (WDC) na kupitishwa

na timu ya wataalam wa Halmashauri, ikizingatiwa kwamba mjumbe huyo atakuwa madarakani kwa kipindi kilichobaki cha mtu yule ambaye nafasi yake imechukuliwa.

(4) Mjumbe aliyeteuliwa chini ya kifungu kidogo cha 3 hapo juu anaweza kuchaguliwa katika uchaguzi mwingine

(5) Pale ambapo Bodi au kamati nyingine yoyote ilianzishwa na hati hii inakufa, wajumbe wote wa Bodi au kamati iliyokufa watasitishwa uanachama na watapoteza nafasi zao.

Bodi na uwezo wa kukagua

38. Bodi kupitia Halmashauri, itakuwa na madaraka ya kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa huduma za afya zinazotolewa kwenye eneo la Halmashauri.

SEHEMU YA VI
MICHANGO YA ADA YA UANACHAMA

Kiwango cha Mchango au Ada ya Mwanachama.

39. (a) Mtu yeyote atakayetaka kuwa mwanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii atapaswa kulipa kila mwaka mchango wa kiasi cha Shilingi Elfu Kumi tu (10,000/=) kwa kila Mtu mwenye umri zaidi ya miaka mitano (5);

(b) Viwango hivi vinaweza kufanyiwa marekebisho na Halmashauri wakati wowote iwapo itaonekana kuna umuhimu wa kufanya marekebisho hayo;

Muda wa Uanachama

40. (a) Mtu yeyote atabaki kuwa mwanachama wa mfuko wa afya ya jamii kila atakapolipa ada yake ya mwaka ya uanachama; na

(b) Kila mwaka unapoisha Uanachama wa mtu utafikia mwisho hadi pale atakapotimiza masharti ya kifungu (a) hapo juu.

Malipo ya Papo kwa Papo

41. (1) Mtu yeyote ambaye hatakuwa Mwanachama wa Mfuko huu atalipa malipo ya papo kwa papo kila atakapoenda kupata matibabu katika Kituo cha kutolea Huduma za Afya.

(2) Malipo ya Papo kwa Papo yatalipwa kwa ajili ya huduma zote za afya zitolewazo kama ifuatavyo:-

(a) Shilingi 2,500/= (Elfu Mbili Mia Tano tu) katika huduma za Afya zinazotolewa na Zahanati katika eneo lolote la Halmashauri;

(b) Shilingi 5,000/= (Elfu Tano tu) kwa huduma za afya zinazotolewa na kituo cha afya kilichopo ndani ya Halmashauri; na

(c) Huduma za hospitali za aina zote ni kulingana na sera ya uchangiaji.

Utaratibu wa Misamaha

42. Misamaha kwa wasioweza kulipia gharama za matibabu utatolewa na kulipiwa na Halmashauri baada ya kuzingatia utaratibu ufuatao:-

(a) Serikali ya Mtaa katika vikao vyake itawatambua, kuwajadili na kupeleka kwa Kamati ya Maendeleo ya Kata mapendekezo ya orodha ya majina ya watu wanaostahili kupewa Msamaha;

(b) Kamati ya Maendeleo ya Kata itawajadili wale wasioweza kulipia gharama na kuthibitisha orodha yao na kuiwasilisha kwa Bodi; na

(c) Bodi ya afya itapokea na kujadili mapendekezo husika na kuyawasilisha pamoja na gharama zake kwa Halmashauri kwa ajili

ya kulipiwa.

Utoaji wa Kadi kwa Mwanachama

43. (1) Kila mwanachama wa Mfuko atapewa Kadi baada ya kulipa mchango wake wa mwaka wa shilingi 10,000/= (Elfu Kumi tu).

(2) Kwa kuzingatia Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii Sura ya 409 kila mtu atakayesamehewa kulipa mchango atapewa Kadi ya uanachama na Halmashauri italipa gharama ya kadi hiyo.

Makosa na Adhabu

44. Mtu yeyote ambaye:-

(a) Atakwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi;

(b) Atafanya kitendo chochote ambacho kitazuia Bodi kufanya kazi zake kwa ufanisi;

(c) Atatumia vibaya mali na rasilimali za Mfuko;

(d) Atashindwa kwa uzembe kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

(e) Atazuia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi; na atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi 50,000/= (Elfu Hamsini) au kifungo cha miezi kumi na miwili (12) au vyote viwili yaani faini na kifungo.

Nembo ya Halmashauri imewekwa katika Sheria Ndogo hizi kwa kuzingatia Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Halmashauri uliiofanyika tarehe 04 mwezi 08 mwaka 2014, Mbele ya:

ABDALLAH IDD MFAUME,
Mkurugenzi
Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe.

VINCENT BENEDICTO BUSIGA,
Mwenyekiti
Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe

NAKUBALI,

Dodoma,
03 November, 2015

MHE. MIZENGO P. PINDA (MB.)
Waziri Mkuu